HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE | DESEMBA 2024 | HALIUZWI

Jarida la

# TEMEKE YETU

FAHAMU ZAIDI

## Zahanati ya Kilakala Yapandishwa Hadhi Kuwa Kituo cha Afya



TOLEO LA 09

## MABADILIKO YANAANZA SASA

"Serikali ina Majukumu makubwa mawili, Jukumu la kwanza ni Utawala na la pili ni kuwaletea Wananchi Maendeleo. Wajibu wetu Sisi Viongozi ni kukidhi matarajio ya Wananchi kwa Serikali yao..."

Temeke Municipal Council

Scan hapa kusoma toleo lililopita. Au, Pakua katika tovuti yetu ya www.temekemc.go.tz

HISTORIA YA YA TEMEKKE

Manispaa ya Temeke ni moja ya Halmashauri chache kongwe zenye utajiri na historia ambayo imechangia kuleta mabadiliko kisiasa, kiuchumi na kijamii Nchini. Kwa ujumla Temeke imekuwa kitovu cha upatikanaji wa uhuru wa Tanzania bara, pia kwa ukuaji wa michezo, utamaduni na maendeleo ya kilimo katika jiji la Dar es Salaam.

Manispaa ya Temeke ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 240 iliundwa 1999 chini ya sheria ya Serikali za mitaa (mamlaka ya miji) ya mwaka1982

Manispaa ya Temeke ipo kusini mwa mkoa wa Dar es salaam ambapo Mashariki inapatikana Bahari ya Hindi, Kusini inapakana na wilaya ya Mkuranga iliyopo mkoa wa Pwani na Kaskazini-Magharibi imepakana na manispaa ya Ilala wakati kwa upande wa Kaskazini-Mashariki Halmashauri hii imepakana na halmashauri ya manispaa ya Kigamboni.

Temeke ina majimbo makuu mawili ya uchaguzi (Temeke na Mbagala) ina idadi kubwa ya watu ambapo kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 idadi ya watu ni 1,346,674 kati yao wanawake ni 691,537 na wanaume ni 655,137.

Temeke ni moja ya Wilaya inayolibeba Jiji la Dar-es-Salaam, kivipi, Dar-es-Salaam ni Temeke kwa kuwa bandari ipo Temeke,viwanja vyote vya mipira kitaifa - Uwanja wa Taifa na uwanja wa Uhuru, pia ipo jirani na Uwanja wa ndege wa kimataifa, ni mwanzo wa Reli ya Tazara, ina Uwanja wa kimataifa wa maonesho - sabasaba, ina daraja la Nyerere ambalo ni la Kimataifa. Samaki hupatikana kwa uwingi Temeke, ina fukwe nzuri za kuvutia zenye mchanga mweupe, ina wakazi wengi na wahamiaji wanaopata maeneo ya kujenga kutokana na kuwa na maeneo makubwa tena ya wazi. Ina mtandao mkubwa wa barabara za lami. Hii ndiyoTemeke tunayoisema.



Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022, idadi ya wakazi wake ni 1,368,881 kati ya hao wanawake 699,825 na wanaume 669,056. Kijiografia Temeke ina ukubwa wa Kilomita za mraba 240 baada ya kugawanywa na kuzaliwa Wilaya mpya ya Kigamboni, Kwa upande wa Mashariki, Temeke imepakana na bahari ya Hindi, Kusini kuna Wilaya ya Mkuranga na Magharibi kusini kuna Wilaya ya Ilala kwa kufuata reli ya kati.

Manispaa ya Temeke ni lango la kuingia kutoka Nchi za Kusini mwa Afrika zikiwemo Msumbiji, Afrika ya Kusini n.k kupitia upande wa Kusini upande wa Kaskazini kuna Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere hivyo ni rahisi kwa wawekezaji kufanya biashara za Kimataifa.

Ndg. Jomaary Mrisho Satura,
Mkurugenzi Manispaa ya Temeke

## Timu ya Utayarishaji


### Mhariri Mkuu

**Joanita Joseph**
*Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,*
*Manispaa ya Temeke*

### Wahariri Wasaidizi

**Mussa Chisongela**
**Sweetbetter Njige**
**Rehema Isango**

### Msanifu wa Jarida

**Simon Joshua**

### Wapiga Picha

**Gervas Edick**
**Shamsi Mustapha**
**Simon Joshua**

*Jarida hili hutolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,*
*Halmashauri ya Manispaa ya Temeke*
*S.L.P 46343 Temeke, Dar es Salaam*
*Simu: +255 22-2928132, Nukushi: +255 22-2928137*
*Baruapepe: temeke@temekemc.go.tz*
*Tovuti: temekemc.go.tz*



# Majaliwa Afanya Ziara Temeke, Akagua Miradi na Kutoa Maagizo

Na Mwandishi Wetu,
TMC Habari.

Waziri mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mheshimiwa Kassim Majaliwa amefanya ziara wilaya ya Temeke na kuzungumza na watumishi wa umma juu ya masuala mbalimbali ya kiutendaji pamoja na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya manispaa.

Katika ziara hiyo waziri mkuu Majaliwa amefungua bwalo la chakula na bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 230 wa kidato cha tano na sita katika shule kongwe ya sekondari Kibasila. Amesema

"Nimefurahi sana kuja Kibasila. Panapendeza, hongera sana. Wanafunzi, walimu na watumishi wasio walimu, ziara hii inanipitisha kwenye maeneo ambayo fedha ya Serikali imeletwa kwa ajili ya kujenga majengo maalum kwa ajili ya matumizi ya Wananchi. Kupitia serikali ya awamu ya sita Sekta ya elimu imeendelea kuboreshwa, kila eneo limeendelea kujenjwa ila kazi ya kujifunza na kufundisha iendelee vizuri.

Tumepata matatizo mengi kwa vijana kutokana na kukaa mbali utulivu wa kujisomea unapotea. Rais Dokta Samia ameelekeza halmashauri zote waone mahitaji ni nini ili mahitaji yatekelezwe.

Tumejenga madarasa sasa ni zamu ya mabweni. Wasichana wana upendo sana, wakitoka shule wanaenda kufanya kazi kusaidia hamna muda wa kusoma ili kuzuia haya, tunajenga mabweni kama haya. Bweni ni zuri la kisasa safi kabisa tayari kwa matumizi

Wito wangu kwenu ni lazima tuuliende mradi huu. Tunzeni miundombinu yote ili tutumie muda mrefu. Simamieni usafi na usalama kwa vijana kwenye maeneo yetu haya".

Aidha waziri mkuu Majaliwa amehutubia Wananchi wa Temeke na kuwakumbusha nia njema ya Serikali ya awamu ya sita katika kuleta maendeleo kupitia uwekezaji na uendelezaji wa miradi mbalimbali. Alisema

"Mradi wa mwendokasi wa Bilioni 189 upo 98%, tukishakamilisha tunaanza kutiririsha mabasi, tayari tumeshatafuta mzabuni ameshaagiza mabasi na yakifika hapa mradi unaanza mara moja. Hospitali ya ghorofa 6 ya Mbagala rangitatu iliyotugharimu bilioni 10.8 itakamilika haraka, nimepita hapo, nimekagua na nimewaambia waongeze kasi ili Wananchi wapate huduma"

Katika ziara hiyo Majaliwa amuagiza mkurugenzi wa manispaa ya Temeke Jomaary Satura kuhakikisha barabara kuu zinawekwa taa zitakazo mulika nyakati za usiku ili kupendezesha mji na kuongeza usalama kwa raia.

# Majiko ya Gesi 800 Yakabidhiwa Bure Temeke

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.



Katika kuunga mkono jitihada za kinara wa ajenda ya nishati safi ya kupikia Nchini na barani Afrika mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, mstahiki meya wa manispaa ya Temeke mhe. Abdallah Mtinika ameongoza zoezi la ugawaji wa majiko ya gesi 800 bure kwa wakazi wa manispaa ya Temeke.

Akiongoza zoezi hilo mheshimiwa Mtinika ameeleza umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla huku akiweka msisitizo mkubwa katika kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia Nchi.

Aidha mhe. Mtinika ameeleza kuwa manispaa ya Temeke imejipanga kumuunga mkono mhe. Rais kwa kuweka mpango wa matumizi ya nishati safi.
“Mheshimiwa Rais anayo nia njema na maono ya kuleta mabadiliko kwa mazingira yetu na kwetu binafsi, mama zetu wameumwa macho, vifua, mapafu kwasababu ya mkaa na kuni. Dunia imebadilika kimazingira kutokana na uchomaji wa mikaa (ukataji miti kiholela) maisha ya sasa yamebadilika gesi sio anasa tena ni hitaji muhimu na tupo hapa kufanikisha hilo kwa ajili yetu na mazingira yetu

Sisi kama halmashauri tumetoa pesa kununua majiko 800 kwa mwaka huu wa fedha lakini bado tutaendelea kumuunga mkono Rais wetu kwa kuweka utaratibu sahihi wa kufikia matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa 100%”.

Kwa upande wake afisa maendeleo ya jamii na mratibu wa uwezeshaji Wananchi kiuchumi bi. Glory Magushani amesema lengo kuu la ugawaji wa majiko hayo ni kuhamasisha makundi mbalimbali katika jamii.

SOMA MATOLEO MENGINE YA JARIDA LA TEMEKE YETU KUPITIA TOVUTI YA TEMEKEMC.GO.TZ









# Temeke Yapokea Hundi ya Bilioni 9.4 mikopo ya 10% Makundi Maalum

Na Joanita Joseph,
TMC Habari.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Albert Chalamila leo Desemba 05, 2024 ameikabidhi Manispaa ya Temeke hundi ya Shilingi Bilioni 9.4 katika Hafla ya Uzinduzi wa Ugawaji wa Vitambulisho vya Kidijitali kwa Wafanyabiashara ndogondogo na Mikopo ya 10% inayotokana na Mapato ya ndani ya halmashauri kwa kundi la Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Akizungumza katika Hafla hiyo RC Chalamila ametoa Maagizo kadhaa ikiwemo wadaiwa wote waliochukua mikopo hii kwa awamu zilizopita haraka madeni yao.

"Natoa maagizo kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya, watu hawa waliochukua mikopo ya halmashauri isiyo na riba, jasho la watanzania, wakamatwe haraka wapelekwe Mahakamani. Tusipende kuchezea Uchumi wa Taifa" alisema RC Chalamila.

Vilevile RC Chalamila ameiagiza Taasidi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kushughulika na Viongozi wanaofanya hujuma katika Mikopo hiyo


"Naiagiza TAKUKURU ikaangalie Viongozi wanaodanganya na kutapeli Wafanyabiashara wakachukue fedha na kisha kuwanyang'anya fedha hizo, lakini pia ma 'consultant' muwasaidie wafanyabiashara hawa kuwekeza kwenye maeneo sahihi ili pesa izunguke na hili litawawezesha kulipa mikopo hii"

RC Chalamila amekemea ubaguzi katika utoaji wa Mikopo hii na kusisitiza kuangaliwa kwa Vigezo.

"Mikopo hii si ya CCM peke yao ni ya CUF, Chadema, UDP, bali ni ya kila Mtanzania aliye chini ya Uongozi wa Dr. Samia msiende kutoa mikopo kwa ubaguzi kwa kuuliza itikadi, ukanda...Msibague watu katika kuwapatia mikopo".

Aidha RC Chalamila amewataka wafanyabiashara kuondoka Barabarani na kufanya biashara katika maeneo yaliyo rasmi.

"Mji huu unataka usafi, huwezi kupangabiasharakilasehemukila mahali, tupange upya biashara zetu. Tusisubiri kusimamiwa tupange miji yetu vizuri, juzi tu kariakoo kupitisha vifaa vya uokoaji ilikuwa shida, biashara zimepangwa kila sehemu.



# Bilioni 50 Kuboresha Miundombinu Manispaa ya Temeke (DMDP II)

Na Joanita Joseph,
TMC Habari.

Leo Oktoba 24, 2024 Historia mpya imeandikwa katika Nchi Yetu hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) katika Viwanja vya Mwembeyanga Temeke ameshuhudia Utiaji Saini wa takribani Mikataba 8 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 190 (190,040,361,931.41) kwa ajili Ujenzi wa Barabara na Miundo mbinu muhimu katika halmashauri zote tano Jijini Dar es Salaam kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili (DMDP Phase Two)

Akizungumza katika hotuba Yake Mhe. Mchengerwa amesema

'Ujenzi wa mindombinu hii hakikisheni inazingatia thamani ya fedha na mahitaji ya Wananchi, tunapokwenda kwenye Ujenzi wa Masoko hakikisheni Masoko haya yawe ni yale yenye uhitaji kwa wananchi'

Miongoni mwa Mikataba hiyo Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imepata mitakaba 2 yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 50,025,554,462 kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara zenye Urefu wa Km 13.04.

Barabara hizo ni Nduguru 1.64 km, Masako 3.91 km, Maandazi 2 km, Madaraja ya Miguu (Chaurembo 1 na 2), Songambele 0.32 km, Mwakalinga 1.07 km, Markas 0.48 km, Majimaji 0.32 km, Magorofani 0.31km, Igome/Yemen 0.85 km, Diwani 0.67 km, Keko Machungwa 0.57 km, na Basri O.9 km ambapo zote zitajengwa na Mkandarasi CRJE (EA) Ltd.

Mradi wa DMDP Awamu ya Pili uliobeba thamani ya Dola Milioni 438 za Marekani ni muendelezo wa yaliyofanywa katika Awamu ya Kwanza ya mradi huo katika Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam.

Uboreshaji na Ujenzi wa Miundombinu Muhimu utahakikisha Wananchi wote wa Temeke wanapata huduma bora, ambapo kwa Awamu hii ya Pili Mradi huu unatarajia kuboresha Mtandao wa Barabara manispaa hapo kwa Zaidi ya kilomita 250, kilomita 90 za mifereji mikubwa ya maji ya mvua, vituo 9 vya mabasi, masoko 18 na madampo matatu ya Kisasa.



# MATANGAZO










JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

## LIPA USHURU WA HUDUMA ZA HALMASHAURI (SERVICE LEVY)

Wafanyabiashara wote mnakumbushwa kulipa ushuru wa huduma (Service Levy).

Ili kupata namba ya Malipo (Control Numbers) fika Ofisi za Mapato za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke au fika katika vituo vya kutolea huduma (Clusters) vilivyopo katika Ofisi kata za Miburani, Charambe, Buza, Kijichi, Tandika na Chamazi.

www.temekemc.go.tz

Miaka ya Uhuru 63 WA TANGANYIKA




# Dkt. Samia Kutengeneza Mazingira Wezeshi kwa Wazalishaji

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Leo Oktoba 2, 2024 Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Suleiman S. Jaffo ameongoza hafla fupi ya kufunga Maonesho ya Kimataifa ya Viwanda (TIMEXPO) yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwl. Nyerere (Sabasaba) Temeke, Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo Waziri Jaffo amesema ni fahari kwa Watanzania kuzalisha, kusambaza na kutumia bidhaa zilizozalishwa ndani ya Nchi na kuwa Serikali imejipanga kuboresha mazingira kwa wazalishaji ili kuimarisha biashara na ajira. Amesema

"Watanzania tuamke, tujivunie vya kwetu, nimeona fahari sana kukagua bidhaa na zimeandikwa 'made in Tanzania'...Serikali ya Rais Samia inaendelea kutengeneza mazingira wezeshi kuhakikisha uwekezaji wa viwanda na uchumi unaenda vizuri. Sisi kama watendaji, tutajitahidi kupitia mambo yenye kuleta changamoto kubwa yanatatuliwa ili kuhakikisha bidhaa za ndani zinapata masoko kwa ajili ya kutunza ajira na uendelevu wa viwanda hivi"

Aidha Mhe. Jaffo amewapongeza wazalishaji wote ikiwemo wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuzalisha ajira kwa vijana kama lilivyo lengo la sekta binafsi ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mkuu wa Wilaya ya Temeke mhe. Sixtus Mapunda amesema;
"Nawashukuru waandaji wa maonesho haya CTI (Confederation of Tanzania Industries) na Mamlaka ya maendeleo ya biashara Tanzania (Tantrade) kwa maonesho mazuri, naamini Temeke tutaendelea kuwa wenyeji kwa maonesho haya ambayo naamini yatakuwa ya pili kwa ukubwa baada ya yale ya sabasaba".

Maonesho ya kimataifa ya viwanda yamefanyika mara ya pili na kwa mafanikio makubwa kutokaka kuwa na washiriki 79 mwaka 2023 kufikia washiriki 257 mwaka 2024.

## Fikra za Satura



**"Serikali ina Majukumu makubwa mawili, Jukumu la kwanza ni Utawala na la pili ni kuwaletea Wananchi Maendeleo. Wajibu wetu Sisi Viongozi ni kukidhi matarajio ya Wananchi kwa Serikali yao....sasa hapa kwenye matarajio ndipo kama Kiongozi unaangalia timu uliyonayo, Je inakidhi matarajio? Ninaamini ninyi ni timu ya Ushindi, Tufanye kazi!".**

**- Jomaary Mrisho Satura**
**Mkurugenzi Manispaa ya Temeke**




*Chuo cha Uuguzi na Ukunga kilichopo Kata ya Mbagala Charambe, Manispaa ya Temeke kilichofungiwa kutokana na kukosa sifa na mazingira wezeshi ya mwanafunzi kujisomea. Chuo hicho kimefungiwa kwa muda usiojulikana.*

# DC Mapunda Akipiga 'STOP' Chuo cha KEWOVAC

Na Joanita Joseph,
TMC Habari.

Ikiwa ni Siku 5 zimepita toka Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe. Sixtus Mapunda kutoa agizo la kusitishwa kwa Mafunzo katika Chuo cha Kewovac kilichopo Mbagala Charambe kinachojihusisha na utoaji wa elimu ya uuguzi na ukunga.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) limetoa Rai kwa Wananchi kuchukua tahadhari wanapowatafutia watoto wao nafasi za masomo kwenye Vyuo vinavyojitangaza kutoa elimu.

Rai hiyo imetolewa Novemba 24, 2024 na Meneja Uthibiti Ubora NACTVET Mhandisi Enock Kayani pamoja na timu yake mara baada ya kufanya Ukaguzi wa maeneo ya Chuo hicho kilichogundulika kutosajiliwa na kukosa Mtaala, miundombinu yenye kukidhi sifa za kutoa Mafunzo ya uuguzi na ukunga pamoja na kuwa na mazingira hatarishi kwa wanafunzi wake.

"Mhe. DC alifanya vyema kukifungia Chuo hiki, sisi kama Taasisi inayojihusisha na Ubora wa elimu ya Ufundi na Mafunzo ya ufundi stadi tunaona kabisa kuna tatizo" alisema Mhandisi Kayani.

Mhandisi Kayani amewasihi wazazi kujiridhisha kwanza na usajili wa vyuo kabla ya kuwapeleka watoto wao kuchukua mafunzo sambamba na kuwatka wazazi wenye watoto chuoni hapo kuwaondoa mara moja.



# Kamati ya Lishe Temeke Kuja na Tamasha la Magonjwa Yasiyoambukiza

Na Shamsi Dady,
TMC Habari.

Leo Novemba 11, 2024 kamati ya lishe halmashauri ya manispaa ya Temeke imefanya kikao cha robo ya kwanza (Julai-Septemba 2024-2025) kujadili mafanikio pamoja na changamoto mbalimbali za masuala ya lishe ikiwemo eneo la afya ya mama na mtoto.

Akizungumza katika kikao hicho Mkuu wa wilaya ya Temeke kumaliza kabisa magonjwa yatokanayo na lishe kwa mama na mtoto. Amesema

"Muda uliowekwa wa kuanza kutoa huduma ya chanjo kwa mama na mtoto mpaka kufikia mwezi Mei, 2025 itakuwa mbali punguzeni ili kuwezesha huduma hii kufikiwa kwa haraka zaidi na itapendeza zaidi mkitengeneza misingi mizuri ya watu kujitokeza kwa wingi katika vituo mtakavyopanga". Alisema Mhe. Sixtus Mapunda.

Kwa upande wake mratibu wa kuweka mikakati ya kuboresha hali ya lishe ndani ya manispaa kwa kushirikiana na wadau na jamii husika.

"Tumeandaa kongamano la maadhimisho ya wiki ya magonjwa yasiyoambukiza ambapo tutahusisha elimu ya lishe,uchunguzi wa magonjwa kama shinikizo la damu,kisukari,tezi dume,saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti kuanzia Novemba 14-15 mwaka huu karibuni sana hapa hapa manispaa ya Temeke".



Mhe. Sixtus Mapunda ameagiza kamati ya lishe kuhakikisha utafiti wa viashiria vya magonjwa yanayohusiana na lishe pamoja na chanjo kwa mama na mtoto ufanyike haraka ili kudhibiti na lishe bi. Happy Nkunda ameeleza lengo la kikao hicho kililenga kukagua na kupitia viashiria kuanzia ngazi ya kata na ngazi ya halmashauri na kubainisha changamoto, mafanikio na Manispaa ya Temeke inaendelea kutekeleza kikamilifu mkataba na makunaliano ya lishe kuanzia ngazi ya chini (kata) kwa kushirikiana viongozi na wadau muhimu wa maendeleo.

# Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wapewa Mafunzo ya Uongozi

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Baada ya uchaguzi wa Serikali za mitaa uliofanyika Novemba 27, 2024 na zoezi la uapisho kufanyika, Wenyeviti wa Serikali za mitaa yote 142 ya manispaa ya Temeke wameshiriki mafunzo ya uongozi yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Idd Nyundo.

Akifungua mafunzo hayo Mstahiki meya mheshimiwa Abdallah Mtinika amewataka Wenyeviti kuwa na umoja, mshikamano na maelewano na viongozi pamoja na watendaji wengine. Alisema

"...Nimepokea changamoto zenu na tumekubaliana kuzifanyia kazi kwa utaratibu mzuri....tutambue kuwa tuko hapa kujenga nyumba moja, imara. Ujenzi sio kazi nyepesi na ni hatua lakini huwezi kusema hili paa limekosewa sana siwezi kuendelea kujenga, hapana, tunakosea, tunasimama tena hatimaye tunainua nyumba imara pamoja.

Akitoa mafunzo hayo mhadhiri kutoka chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) maarufu kama Hombolo ndugu Jonas Kapwani amewaeleza Wenyeviti kupitia somo la Uongozi na Utawala bora kuwa nafasi zao ni kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wanapaswa kufuata muongozo wa katiba katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku

"Uongozi ni dhamana, unapaswa kuwa mtiifu na mnyenyekevu badala ya kuwa mwenye mamlaka.



## Habari Picha



*Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe.Sixtus Mapunda leo Oktoba 31, 2024 ameshiriki Mahafali ya kuhitimisha Mafunzo kwa Jeshi la Akiba akiwa Mgeni rasmi akimuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila.*

*Mahafali hayo yaliyohudhuriwa na Viongozi mbalimbali yamefanyika katika Viwanja vya Uhuru, wilayani Temeke na jumla ya Wahitimu 470 wamehitimu mafunzo hayo.*

# Temeke Yafanya Bonanza Kuhamasisha Uchaguzi Serikali za Mitaa

Na Joanitha Joseph,
TMC Habari.

Ikiwa zimebaki siku 3 kufikia Novemba 27, 2024 siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa leo Novemba 24, 2027 katika Viwanja vya Mwembeyanga Manispaa ya Temeke imefanya Bonanza kubwa Mahsusi kwa ajili ya kuhamasisha Wananchi hususani Wakazi wa Temeke kujitokeza kupiga kura siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuchagua Viongozi Bora.

Katika Bonanza hilo Wananchi wamepata fursa ya kupatiwa elimu ya mpiga kura pamoja na Matumizi sahihi ya Nishati safi hususani gesi na kuachana na matumizi ya Mkaa na kuni ili kuepukana na uharibifu wa Mazingira na Magonjwa yanayosabishwa na uvutaji wa hewa chafu.

Akizungumza katika Viwanja vya Mwembeyanga, Mkuu wa Wilaya ya Temeke ambaye pia alikuwa ni Mgeni rasmi katika Bonanza hilo amesema

"Tarehe 27 kila mmoja akiache kitanda chake kama leo, Amgongee na jirani yake tukapige kura" Alisema DC Mapunda

Bonanza hilo lililosheheni Burudani kabambe kutoka kwa Wasanii wa Muziki wa Kizazi kipya na Vikundi vya Ngoma za asili limehudhuriwa na Viongozi mbalimbali, Chama cha Mbio za Pole Temeke yaani Temeke Jogging Association (TEJA), Vikundi mbalimbali vya Mbio za pole, Wajasiriamali pamoja na Wadau mbali mbali wa Afya na Nishati safi.

***'Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze kushiriki Uchaguzi".***





*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wanafunzi wenye mahitaji malum Kibasila wakimsikiliza kwa makini Afsa Elimu Maalum Manispaa ya Temeke, Bi. Martha Kusaga shuleni hapo alipowatembelea kwa ajili ya elimu ya kujitambua.*

# Idara ya Elimu Sekondari yakutana na Watoto wenye Mahitaji Maalum

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kupitia Idara ya Elimu Sekondari imekutana na wanafunzi wenye mahitaji maalum kutoka Shule za Sekondari za umma zilizopo katika Manispaa ya Temeke lengo likiwa ni kufanya maboresho katika mahitaji yao.

Akizungumza katika Mkutano huo Afisa Elimu anayeshughulikia elimu maalum Bi. Martha Kusaga amefafanua juu ya utofauti wa aina za mahitaji na namna ya kuyafikia ikiwa ni pamoja na kupokea maoni ya Wanafunzi hao na kuweka maazimio yatakayotekelezwa.

"Mfano wa mahitaji maalum kwa wanafunzi hawa ni pamoja na ongezeko la muda katika mitihani (au kupata usaidizi kutokana na aina ya ulemavu) au kuweka/kuboresha aina ya miundombinu inayohitajika. Hivyo, tunakutana ili viongozi wajue mahitaji yenu" alisema Bi. Martha.

Aidha ameeleza kwamba wameazimia kuwa kila shule iwe na walimu wasimamizi wa mahitaji maalum ili kusikiliza na kutatua changamoto za wanafunzi hao pamoja na kutenga siku maalum ya kukutana na kuzungumza nao.

"Mungu anatambua uwepo wenu, hali kadhalika Serikali yenu inatambua uwepo wenu, nanyi naomba mtambue uwepo wenu na kusudi lenu la kuwepo hapa," alisema Bi. Martha

*"Mungu hajakosea kutuumba tulivyo, tujikubali na kujipenda..."*

"Mungu hajakosea kutuumba tulivyo, tujikubali na kujipenda ili tuishi kwa furaha"
Mkutano huo umefanyika katika Shule ya Sekondari Kibasila ambapo wanafunzi hao pamoja na kueleza changamoto zao walipata wasaa wa kuonesha pia vipaji vyao na kupata burudani mbalimbali ikiwemo kuimba wimbo wa Taifa kwa alama na kucheza.

# Temeke Yaadhimisha Wiki ya Elimu ya Watu Wazima

Na Sweetbetter Njige
TMC Habari.



Leo Oktoba 4, 2024 manispaa ya Temeke kupitia idara ya elimu msingi imeadhimisha juma la elimu ya watu wazima katika viwanja vya Zakhem- Mbagala na kuhimiza fursa ya elimu kwa wote.

Akizungumza kwa niaba ya mgeni rasmi, mkuu wa wilaya ya Temeke, Afisa tarafa ya Mbagala Betha Minga amesema kuwa Serikali ya awamu ya sita imelenga kuboresha elimu kwa watu wazima ili kutoa fursa kwa wote.

"Lengo la Serikali ni kuifanya elimu kuwa jumuishi kwa makundi yote. Hii ni kwa watu wazima na wale ambao walipata ujauzito shuleni wakakatisha masomo bado wanayo fursa ya kurudi shule kusoma. Tunajua umuhimu wa watu kujifunza stadi mbalimbali licha ya kuwa nje ya mfumo rasmi wa elimu. Nimeona baadhi ya maafisa maendeleo hapa, ile 4% ya mikopo kwa vijana tuwaangalie na hawa kwa sababu tayari wana ujuzi na wanaaminika".

Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi mratibu wa elimu ya watu wazima manispaa ya Temeke Noconia Yusufu amesema maadhimisho hayo yanalenga kuimarisha uratibu, usimamizi na kuthamini maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi.

Maadhimisho ya juma la elimu ya watu wazima huazimishwa na Nchi mbalimbali Duniani ambazo ni wanachama wa UNESCO, huungana katika kupima na kutafakari mafanikio na changamoto zilizopo katika utoaji wa elimu ya watu wazima nchini Tanzania.





# Temeke Kukagua Vikundi vya Wanufaika wa Mikopo ya 10% Kabla ya Uhakiki

Na Mwandishi Wetu,
TMC Habari.

**Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Bi. Furaha Chiwile, leo Desemba 11, 2024, ameongoza kikao cha ukaguzi wa** awali wa vikundi vinavyotarajiwa kupatiwa mikopo ya 10% kutoka kwenye mapato ya ndani ya manispaa hiyo. Mikopo hiyo inatolewa kwa makundi maalum ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa vikundi vinavyonufaika vinakidhi vigezo kabla ya kufikishwa kwenye Kamati ya Mikopo ya Wilaya kwa uhakiki wa mwisho.

Katika kikao hicho, jumla ya vikundi 160 kutoka mitaa yote 142 ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke vilifanyiwa ukaguzi wa awali. Ukaguzi huu ni sehemu muhimu ya mchakato wa utoaji wa mikopo, ukilenga kuthibitisha uhalali wa vikundi, uendelevu wa shughuli zao, na uwezo wao wa kutumia fedha kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa kufanya hivyo, halmashauri inahakikisha kuwa mikopo hii inaleta athari chanya kwa walengwa na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Manispaa ya Temeke.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika katika Ukumbi wa Iddy Nyundo, Bi. Chiwile amesisitiza kuwa vikundi vinapaswa kuzingatia masharti yote ya mikopo ili kuhakikisha fedha wanazopatiwa zinatumika ipasavyo. Pia, alihimiza ushirikiano kati ya wanavikundi na maafisa wa maendeleo ya jamii kwa lengo la kuboresha mifumo ya ufuatiliaji wa mikopo na kuhakikisha urejeshaji wa fedha kwa wakati. Alibainisha kuwa utaratibu huu unalenga kuongeza uwajibikaji na kuhakikisha kuwa mpango wa mikopo unaendelea kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Kwa upande wake, baadhi ya wanavikundi walioshiriki katika kikao hicho wameeleza kuwa mikopo ya 10% ni fursa muhimu kwao, hasa kwa wale wanaoendesha biashara ndogo ndogo na miradi ya uzalishaji. Walisema kuwa msaada huu unawasaidia kukuza mitaji yao, kupanua shughuli zao za kiuchumi, na kuongeza fursa za ajira katika jamii. Wameahidi kufuata taratibu zote zilizowekwa ili kuhakikisha wanatumia mikopo hiyo kwa maendeleo yao na jamii kwa ujumla.

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mpango wa mikopo ya 10% unatekelezwa kwa ufanisi. Kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii, wameweka mkazo katika kuwajengea uwezo wanavikundi kuhusu usimamizi wa fedha, ujasiriamali, na mbinu bora za biashara. Mafunzo haya yanasaidia kupunguza hatari ya mikopo kutumika visivyo na kuongeza ufanisi wa urejeshaji wa fedha, jambo linalowezesha mpango huu kuwa endelevu.

Mikopo ya 10% inayotolewa na Halmashauri ni moja ya njia madhubuti za kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupunguza umaskini.

Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa fedha hizi kutumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, huku ikiweka mikakati madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa. Manispaa ya Temeke inaendelea kuhakikisha kuwa kila kikundi kinachonufaika.

# Zahanati Kilakala Yapandishwa Kuwa Kituo cha Afya

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.



Wananchi wa kata ya Kilakala kupitia Diwani wa Kata hiyo Mheshimiwa Amir Salum (Osama) wamemshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya Afya katika Zahanati ya Kilakala iliyowezesha zahanati hiyo kupandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya.

Hayo yamesemwa kufuatia ziara ya mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila wakati akifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo wilaya ya Temeke. Mhe Chalamila amesema.
"Nimpongeze mkuu wa wilaya na mkurugenzi kwa mradi mzuri, marekebisho madogo yapo na nimeelekeza yafanyiwe kazi. Ifahamike, Utejelezaji wa miradi ya afya pamoja na vifaa vyake ni gharama sana.
Uwekezaji mkubwa umefanyika hapa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anampango wa kuleta bima za afya kwa wote ili Wananchi muhudumiwe vizuri. Tunakatia bima magari, tujikatie bima pia, maisha yana thamani kuliko chombo unachotumia leo. Maelekezo ya mhe. Rais ni sisi viongozi kusimamia vyema sekta ya afya".

Zahanati ya Kilakala imeongezewa mejengo tisa ikiwemo jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, jengo la mionzi, walkways, jengo la wagonjwa wa nje (OPD) maabara, nyumba pacha za watumishi, jengo la kufulia, kichomea taka (high taking incinerator) majengo hayo yote yana jumla ya gharama ya shilingi Bilioni 1,009, 334, 356.28 na sasa kimepandishwa hadhi rasmi kuwa kituo cha afya kutoka na ongezeko la miundombinu na huduma zitakazotolewa kituoni hapo.



# RC Chalamila Ahamasisha Vijana na Wanawake Kushiriki Uchaguzi

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

**Kuelekea uchaguzi wa Serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, 2024 mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Albert Chalamila ametoa wito kwa wakazi wa wilaya ya Temeke kushiriki uchaguzi kwa kujiandikisha, kuchagua pamoja na kugombea nafasi za Uongozi.**



Akizungumza na Wananchi katika kituo cha afya Kilakala (Kilichopandishwa hadhi hivi karibuni) mhe. Chalamila amesema baadhi ya Wananchi hawashiriki uchaguzi badala yake hutoa lawama juu ya uongozi bila kuchukua hatua.

“Muda umekaribia, zoezi la kujiandikisha likifika twende tukajiandikishe, vijana na wanawake nawasihi tujitokeze kugombea hizi nafasi kwasababu miongoni mwetu wapo watu ambao kazi yao ni kulaumu, yule mwenyekiti mwizi, yule mjumbe hafanyi kazi yake ukiuliza si ulimchagua anasema hapana, uligombea hapana.

Hamasisheni vijana wanaoweza washiriki kuijenga Tanzania yetu. Shiriki kwa kujiandikisha ili tuwe na matunda mazuri kiasiasa na kiuchumi”.

Aidha mhe. Chalamila ametoa wito kwa wazazi kuzingatia malezi bora kwa watoto hususani ili kuondoa tabia na mlipuko wa matukio yasiyofaa katika jamii.

“Leeni watoto wenu vizuri, hasa kwa wale wazawa. Wafunzeni vijana wenu kuwa na nidhamu. Mtu anaenda kuiba mali ina

> *“Shiriki kwa kujiandikisha ili tuwe na matunda mazuri kiasiasa na kiuchumi”*

thamani ya shilingi milioni 100 anasahau thamani ya maisha yake ni kubwa kuliko hicho anachoiba. Wengine wanashiriki katika matukio maovu ikiwemo utekaji mifano ipo na mnaijua lakini lawama wanabebeshwa Polisi.

Kama tunataka kujenga Taifa letu likiwa salama na imara lazima tuulizane na kujibu maswali ya msingi”.

Mhe. Chalamila amefanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika wilaya ya Temeke na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa bweni na bwalo shule ya sekondari Kibasila, kituo cha afya Kilakala, zahanati mpya ya kurasini na ujenzi wa ofisi ya kata ya Miburani.



# Meya Mtinika Awapokea Washiriki wa Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi

Na Joanita Joseph,
TMC Habari.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke Mhe. Abdallah Mtinika leo Oktoba 30, 2024 amewapokea Washiriki wa Mafunzo ya teknolojia stahiki ya nguvu kazi yanayotolewa katika Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) waliofika katika Manispaa ya Temeke kwa lengo la kwenda kuona na kujifunza kwa vitendo Miradi iliyotekelezwa chini ya Wakala ya Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi.

Akizungumza katika Viwanja vya Manispaa ya Temeke Mhe. Mtinika amesema

'sisi Temeke tumeendelea kuwa walezi na wapokeaji wa jambo hili, mafunzo yenu ni muhimu sana mkimaliza mji 'organize' kwenye vikundi haraka ili muweze kuchangamkia fursa zilizopo katika halmashauri zetu za mikopo ya 10% kwa kundi la Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu zilizopo katika halmashauri zetu ili mje mtumikie Nchi yenu na mfanye malengo yaliyokusudiwa'

Aidha Mhandisi Paul Mhere, Meneja TARURA wilaya ya Temeke amesema

'Serikali inatenga 30% kwa ajili ya makundi maalum yaani vijana, wanawake na walemavu kutumia teknolojia stahiki ya nguvu kazi katika miradi inayotekelezwa, na sisi TARURA tukiwa wadau wa jambo hili tumekuwa tayari na tutaendelea kutoa ushirikiano kwenu ili kuhakikisha tunakuza viwango vyenu kwa manufaa ya Nchi yetu' alisema Mhandisi Mhere.

Miongoni mwa elimu wanazopatiwa Washiriki wa Mafunzo hayo ya muda mfupi katika Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ni pamoja na elimu ya usalama kazini, usafi, ubora, ufunguaji wa kampuni zinazojihusisha na teknolojia ya nguvu kazi stahiki.

Washiriki wa mafunzo hayo kutoka Chuo cha Sayansi na Teknolojia kutoka jijini Mbeya (MUST) wameonesha shauku kubwa katika kujifunza na kutumia teknolojia ya nguvu kazi kama njia mbadala ya kukuza ujuzi na ajira.

Wamesema kuwa mafunzo haya yatawasaidia kuanzisha miradi yenye tija kwa jamii, hususan katika sekta ya ujenzi wa miundombinu kwa kutumia mbinu za kisasa na endelevu.

# Temeke Yaadhimisha Siku ya Lishe

Na Shamsi Dadi,
TMC Habari.



Leo Oktoba 30,2024 Manispaa ya Temeke imeadhimisha siku ya Lishe Kitaifa kwa kutoa Elimu juu ya lishe Bora kwa mama na mtoto.

Akizungumza na Wananchi katika Kata ya mtoni Mhe. Mariamu mtemvu, Diwani Viti maalum Manispaa ya Temeke amewasisitiza akina Mama kuzingatia elimu ya lishe waliopata Kutoka kwa maafisa lishe ili kutengeneza afya bora na imara kwa ukuaji wa mtoto .

"Niwapongeze sana kwa kujitokeza kwa wingi siku ya Leo lakini pia niwasisitize sana, kuzingatia hii elimu tuliopewa na wataalamu wetu ,basi Twende tukayafuate na kuyafanyia kazi kwa faida yetu na watoto wetu. Ninawaomba muende kuwa mabalozi wazuri ,kwa kuwafikishia elimu kwa wale wenzetu ambao hawakupata nafasi ya kujiunga na sisi kwa siku hii,ili jamii nyingi iweze kunufaika na swala la lishe" Alisema Mhe. Mtemvu

Kwa upande wake Afisa lishe wa Manispaa ya Temeke Bi. Happy Nkunda alipata wasaa wa kuzungumza juu ya lengo kuu la kuadhimisha siku ya lishe kitaifa kwa kutoa Elimu juu ya jambo Hilo.

"Lengo kubwa la jambo hili ni kutoa elimu kwa jamii ili kuzingatia mapendekezo ya muongozo wa chakula na lishe kitaifa,na wito wangu kwa wananchi kwamba ili mtoto aweze kuwa na afya mzuri lazima afya ya mama iweze kuzingatiwa kipindi Cha ujauzito". Alisema Bi. Happy Nkunda.

Hafla hiyo imehudhuriwa na maafisa mbalimbali wakiwemo madaktari kutoka vituo mbalimbali vya afya,maafisa ustawi wa jamii wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na wakazi wa Manispaa ya Temeke.



*Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke chini ya Mkurugenzi Ndg.Jomaary Satura leo Oktoba 28, 2024 imetembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika Manispaa ya Temeke.*

*Miradi iliyotembelewa ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya ya Temeke uliopo katika hatua za awali, ujenzi wa Ofisi ya Kata Miburani, Shule ya Sekondari Dovya na Lumo zilizofikia katika hatua za umaliziaji.*



# Faida za Mboga na Matunda kwa Akinamama Wajawazito

Na Mwandishi Wetu,
TMC Habari.




*Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke leo Novemba 16, 2024 imetekeleza kwa vitendo Sera ya Taifa ya Chakula na lishe bora kwa kuwahamasisha na kuwafundisha wakinamama wajawazito na wenye watoto chini ya Miaka mitano juu ya uandaaji wa lishe bora.*
*Mafunzo hayo yamefanyika katika Kituo cha Afya Buza, Manispaa ya Temeke.*

Mboga na matunda ni vyakula muhimu sana kwa afya ya akinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano. Vyakula hivi vina virutubisho muhimu vinavyosaidia ukuaji, kinga ya mwili na ustawi wa jumla wa mama na mtoto. Ulaji wa mboga na matunda husaidia kuimarisha kinga ya mwili kwa kuwa vina vitamini C, E, na A ambazo hulinda mwili dhidi ya magonjwa na maambukizi.Kinga bora ya mwili ni muhimu kwa mama mjamzito na mtoto mchanga kwani husaidia kuzuia maradhi ya mara kwa mara kama vile mafua na homa.

Vyakula hivi pia husaidia ukuaji wa mtoto tumboni na maendeleo yake ya mwili na akili. Folic acid inayopatikana kwenye mboga za kijani kibichi kama mchicha na matembele ni muhimu kwa maendeleo ya ubongo na mfumo wa fahamu wa mtoto, hivyo kusaidia kupunguza hatari ya matatizo ya kimaumbile kama spina bifida. Pia, matunda kama ndizi na maembe yana madini muhimu yanayochangia ukuaji mzuri wa ubongo na kuboresha uwezo wa mtoto kujifunza haraka.

Ulaji wa mboga na matunda husaidia kupunguza hatari ya upungufu wa damu kwa kuwa vyakula hivi vina madini ya chuma ambayo yanahitajika kwa utengenezaji wa seli nyekundu za damu. Kwa mama wajawazito, hili ni muhimu ili kuhakikisha afya bora na kuzuia uchovu wa mara kwa mara. Aidha, vyakula hivi husaidia katika mmeng'enyo bora wa chakula kutokana na uwepo wa nyuzinyuzi zinazopatikana kwenye matunda kama mapapai kuzuia matatizo mbalimbali.

# TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

## MGAWANYO WA MAENEO YA UTOAJI HUDUMA (CLUSTERS)

Halmashauri ya manispaa ya Temeke imesogeza huduma karibu na Wananchi kwa kwa kuanzisha Vituo vya utoaji huduma (Clusters) kwa kuzingatia ukubwa wa eneo lake lenye jumla ya kata 23.

Huduma zitakazotolewa katika vituo hivyo ni pamoja na ulipaji wa ushuru wa huduma (service levy), leseni, huduma za maendeleo ya jamii, kodi za majengo, kodi ya ardhi, huduma za usafi na udhibiti wa taka, huduma za kilimo na uvuvi, huduma za upimaji afya, huduma za usimamizi wa miradi, huduma ya hifadhi ya maliasili na mazingira pamoja na huduma za vibali mbalimbali.

Vituo hivyo vitasaidia kupunguza umbali kwa Wananchi kuja kupata huduma katika Ofisi za Manispaa ya Temeke na Ofisi ya Kata ya Charambe (Kituo cha mapato Charambe) ambapo hapo awali ndizo sehemu pekee zilizokuwa zikipatikana huduma. Huduma zote kwa sasa pia utazipata katika vituo vipya vya kutolea huduma (Cluster).

Hivyo basi Manispaa ya Temeke kwa sasa ina vituo sita (6) vya kutolea huduma ambavyo vinapatikana katika Ofisi za kata ambazo ni kata ya Miburani, Charambe, Tandika, Chamazi, Buza na Kijichi. Na vitahudumia wakazi wa kata zote kwa kuzingatia mchanganuo ufuatao:-

| MIBURANI | CHARAMBE | TANDIKA |
|---|---|---|
| **KATA ZA:**<br><br>CHANG'OMBE<br>MIBURANI<br>KURASINI<br>KEKO<br>TEMEKE | **KATA ZA:**<br><br>CHARAMBE<br>KILUNGULE<br>KIBONDEMAJI<br>MBAGALA<br>KIBURUGWA | **KATA ZA:**<br><br>TANDIKA<br>MTONI<br>AZIMIO<br>SANDALI |
| **BUZA** | **KIJICHI** | **CHAMAZI** |
| **KATA ZA:**<br><br>BUZA<br>YOMBO VITUKA<br>MAKANGARAWE<br>KILAKALA | **KATA ZA:**<br><br>TOANGOMA<br>MBAGALA KUU<br>KIJICHI | **KATA ZA:**<br><br>CHAMAZI<br>MIANZINI |

'Kwa pamoja tushirikiane kujenga Temeke yetu'.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

# LIPA USHURU WA HUDUMA ZA HALMASHAURI (SERVICE LEVY)

Wafanyabiashara wote mnakumbushwa kulipa ushuru wa huduma (Service Levy).

Ili kupata namba ya Malipo (Control Numbers) fika Ofisi za Mapato za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke au fika katika vituo vya kutolea huduma (Clusters) vilivyopo katika Ofisi kata za Miburani, Charambe, Buza, Kijichi, Tandika na Chamazi.

www.temekemc.go.tz

*Jarida hili hutolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,*
*Halmashauri ya Manispaa ya Temeke*
*S.L.P 46343 Temeke, Dar es Salaam*
*Simu: +255 22-2928132, Nukushi: +255 22-2928137*
*Baruapepe: temeke@temekemc.go.tz*
*Tovuti: temekemc.go.tz*